# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

**Na: 35. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini Septemba 1-10, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Septemba 11-20, 2019**



**Muhtasari**


- Unyevunyevu wa Udongo kwa maeneo ya ziwa viktoria na pwani ya kaskazini unatarajiwa kuongezeka kiasi kutokana na mvua za nje ya msimu.
- Maji na malisho ya mifugo yanatarajiwa kuendelea kupungua katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka kutokana na hali ya ukavu.
- Wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka wanashauliwa kuendelea na uandaaji wa mashamba kwa ajili ya msimu wa mvua za msimu zinazotarajiwa kuanza mwezi oktoba 2019.


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBA 1-10, 2019

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita za mwezi Septemba, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika zaidi na ile iliyopo eneo la kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kupungua nguvu. Hali hii iliendelea kuuweka ukanda wa mvua kaskazini zaidi mwa nchi yetu, ilihali uwepo wa mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa uliendelea kusababisha upepo mkali maeneo yote ya ukanda wa pwani. Joto la juu kidogo ya wastani kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilisababisha kuimarika kwa mgandamizo mdogo wa hewa katika eneo hili uliopelekea pepo zenye unyevu kuvuma kuelekea pwani ya kaskazini ya nchi yetu. Hata hivyo, joto la juu kidogo ya wastani katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (Pwani ya Angola) liliendelea kupunguza kasi ya pepo za magharibi kuvuma kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi yetu.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBA 1-10, 2019

Kwa kipindi hicho cha dikadi maeneo mengi ya nchi yalikua makavu isipokua kwa baadhi ya maeneo machache ya ukanda wa Ziwa Viktoria hususan magharibi, kusini na mashariki mwa ziwa Viktoria, mashariki na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma na maeneo ya kati mwa nchi ambayo yamepata vipindi vichache vya mvua. Kiasi cha mvua kilichopimwa ni kati ya milimita 26 hadi milimita 200 kwa maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria na mkoa wa Kigoma na kiasi cha zaidi ya milimita 200 kwa maeneo ya kati ya nchi kama inavyojieleza katika kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Septemba 1- 10, 2019

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBA 1-10, 2019

Katika dikadi ya kwanza ya mwezi wa tisa 2019, hali ya unyevunyevu wa udongo iliendelea kuimarika kiasi katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ukilinganisha na kipindi cha dikadi ya tatu ya mwezi wa nane 2019. Ukanda wa Ziwa Viktoria, nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini taarifa zinaonesha kuwa wakulima walijihusisha zaidi na uandaaji wa mashamba kwa ajili ya msimu wa mvua za vuli unaotarajiwa kuanza mwezi wa kumi 2019. Kuimarika kwa hali

ya unyevunyevu katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria kulisaidiza katika ukuaji wa malisho ya mifugo. Mazao ya Mihogo na viazi vitamu yaliendelea vizuri katika hatua tofauti. Maji na malisho ya mifugo na wanyapori yaliendelea kupungua kiasi kwa maeneo ya kati mwa nchi na nyanda za juu kaskazini mashariki kutokana na hali ya ukavu inayoendelea.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBA 1-10, 2019

Kina cha maji na mtiririko wa maji kwenye mito viliendelea kupungua kiasi kwa maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu na upepo iliyojitokeza.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBA 11-20, 2019

Katika siku kumi zijazo za mwezi Septemba, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu na ile iliyopo eneo la kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuusogeza ukanda wa mvua kuelekea maeneo yanayozunguka ukanda wa Ziwa Viktoria. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha mvua nyepesi katika maeneo ya ukanda wa pwani ya kaskazini hususan katika siku tano za mwanzo ya kipindi hicho. Aidha, joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika maeneo ya pwani ya Angola.

## HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBA 11-20, 2019.

Maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria hususan magharibi (mikoa ya Kagera na Geita,) na mashariki (mikoa ya Simiyu na Mara) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo katika maeneo machache

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), maeneo ya kati mwa nchi (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi), kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mkoa Morogoro). yanatarajiwa kuwa na hali ya ukavu.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa mkoa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) kunatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache hususan katika siku tano za mwanzo za kipindi hicho.

## MATARAJIO NA USHAURI WA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBA 11-20, 2019

Hali ya unyevunyevu katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria na pwani ya kaskazini unatarajiwa kuendelea kuongezeka kiasi kutokana na mvua zinazotarajiwa. Wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka wanashauriwa kuendelea kuandaa mashamba kwa ajili ya msimu wa mvua za vuli unaotarajiwa kuanza mwezi Oktoba 2019. Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua hususan kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) utapelekea kuendelea kupungua kwa maji na matumizi ya binadamu.Wafugaji katika maeneo mengi ya nchi wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu na kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBA 11-20, 2019.

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua kiasi kutokana na hali ya ukavu unaotarajiwa kuendelea. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuwa na matumizi endelevu ya maji.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

*S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz*